# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 992

Jina la Chapisho: Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-811-8

Mtaala huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MTAALA WA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2023
Toleo la Kwanza 2023

ISBN 978-9987-09-811-8

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Mtaala huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

# Yaliyomo

**Orodha ya Majedwali ........................................................................................ iv**

**Vifupisho .............................................................................................................. v**

**Shukurani ............................................................................................................ vi**

**Dibaji ................................................................................................................. viii**

**Sehemu ya Kwanza .............................................................................................. 1**

Utangulizi................................................................................................................ 1

1.1. Usuli ................................................................................................... 1

1.2 Muundo wa Elimu ya Ualimu Elimu ya Msingi ........................................... 2

**Sehemu ya Pili ...................................................................................................... 3**

Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla ................................................................ 3

2.1 Dira .......................................................................................................... 3

2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ............................................................ 3

2.3 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........................................................................ 3

2.3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu .................................................................. 3

2.3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu ...................................................... 4

2.4 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi 4

**Sehemu ya Tatu ...................................................................................................... 5**

Maudhui ya Mtaala .................................................................................................. 5

**Sehemu ya Nne .................................................................................................... 14**

Ufundishaji na Ujifunzaji ....................................................................................... 14

4.1 Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo Chuoni na Shule Jirani ........................... 14

4.2. Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala ........................................................... 15

4.2.1 Rasilimali watu ............................................................................................ 15

4.2.2 Rasilimali vitu na fedha ................................................................................ 15

4.2.3 Rasilimali muda ............................................................................................ 16

4. 3 Lugha ya kufundishia na kujifunzia ............................................................. 19

4.4 Ushiriki wa Wadau katika Utekelezaji wa Mtaala wa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi ...................................................... 19

4.5 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mtaala wa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi ..................................... 19

**Sehemu ya Tano .................................................................................................... 20**

Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ..................................................................... 20

Bibliografia ............................................................................................................ 22

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na.3.1: Maeneo ya Ujifunzaji, Masomo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi. .......... 5

Jedwali Na. 4. 1: Mchanganuo wa muda wa mafunzo kwa masomo ya utaalamu na ya jumla .......... 16

Jedwali Na. 4.2: Mchanganuo wa Muda wa Mafunzo kwa Masomo ya Kufundishia .......... 17

Jedwali Na. 5.1: Alama za upimaji endelevu kwa masomo ya Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji na Ualimu kwa Vitendo .......... 21

Jedwali Na. 5. 2: Alama za upimaji endelevu kwa masomo ya utaalamu na ya jumla. .......... 21

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| WyEST | Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia |

## Shukurani

Maandalizi ya mtaala huu yamehusisha wadau mbalimbali kutoka sekta za umma na binafsi. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha upatikanaji wa Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi. Hivyo, TET inatoa shukurani za dhati kwanza, kwa Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb.). Kamati hiyo ilikuwa na wajumbe kumi (10), wakiongozwa na Mwenyekiti wake Prof. Makenya Abraham Maboko. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi kuhakikisha kuwa mtaala huu unaandaliwa kwa wakati na unakidhi shauku ya wadau juu ya ubora wa elimu ya ualimu.

Pili, shukurani ziende kwa taasisi, wizara na wadau mbalimbali wa elimu walioshiriki kutoa maoni kuhusu uboreshaji wa mtaala. Baadhi ya taasisi, wizara na wadau hao ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wajumbe wa Kamati ya Mapitio ya Sera ya Elimu, wajumbe wa Kamati ya Kufanya Mageuzi Makubwa ya Elimu Zanzibar, viongozi wa dini, Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Taasisi ya Elimu Zanzibar, Bodi na Menejimenti za Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Tanzania, menejimeti na wakufunzi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, Chuo cha Amali Zanzibar, Baraza la Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Ufundi Stadi, Baraza la Mitihani Tanzania, Chama cha Walimu Tanzania, Baraza la Watoto na Vijana Balehe Tanzania. Vilevile, wadau wengine ni wajumbe wa bodi za shule, wanafunzi wa shule za msingi, sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu, walimu wa shule za msingi, sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wahadhiri wa vyuo vikuu, waajiri, wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu, Tume ya Vyama vya Ushirika, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Akademia ya Sayansi Tanzania, Benki Kuu ya Tanzania na Shirika la Chakula na Kilimo la Kimataifa.

Tatu, TET inayashukuru mashirika ya United Nations International Children’s Fund, United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization*, Room to Read, Right to Play, Data Vision, Plan International, Norwegian Refugees Council, Christian Social Services Commission, Global Education Link,* UWEZO*, Hill Packaging Ltd., Teacher*

*Education Support Project, Madrasa Early Childhood Programme–Zanzibar, Morale Foundation for Education and Training na Educate!* kwa kufadhili hatua mbalimbali za uandaaji wa mitaala.

Nne, TET inatoa shukurani za dhati kwa wataalamu wote wa elimu ya ualimu kutoka ndani na nje ya TET walioshiriki kuandaa mtaala huu. Mwisho, ingawa si kwa umuhimu, TET inaishukuru sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST) kwa kuwezesha kazi ya uandishi, uchapaji na usambazaji wa mtaala huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

# Dibaji

Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi umeandaliwa kwa kuzingatia *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023, maoni ya wadau yaliyokusanywa na kuchakatwa mwaka 2021 hadi 2022 na matokeo ya uchambuzi wa maandiko kuhusu uzoefu kutoka nchi nyingine. Aidha, mtaala huu unazingatia dira ya elimu ambayo inalenga kumwandaa Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa. Vilevile, mtaala huu umezingatia malengo makuu ya elimu pamoja na malengo ya elimu ya ualimu nchini Tanzania. Kwa kuzingatia haya, mtaala huu umeweka viwango vya utoaji wa elimu katika ngazi ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu ya Elimu ya Msingi kwa kubainisha maarifa, stadi na mwelekeo atakaoujenga mwalimu tarajali, umahiri wa jumla, maeneo makuu ya ujifunzaji, umahiri mkuu na mahususi, njia na mbinu za ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, mtaala umebainisha muda utakaotumika katika utekelezaji, lugha ya kujifunzia na kufundishia, vifaa vya kufundishia na kujifunzia na njia zitakazotumika katika upimaji wa maendeleo ya mwalimu tarajali kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri. Vilevile, mtaala umebainisha sifa za kitaaluma na kitaalamu za mkufunzi ambaye ndiye mtekelezaji mkuu wa mtaala katika ngazi ya chuo.

Pamoja na matamko mbalimbali ya kisera na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa, mtaala huu umezingatia nadharia za ujifunzaji na Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea. Falsafa hiyo inasisitiza utoaji wa elimu inayomwezesha Mtanzania kujitegemea na kumudu maisha yake ya kila siku. Ni matarajio yangu kuwa kupitia mtaala huu, mkufunzi atamwezesha mwalimu tarajali kujenga umahiri uliokusudiwa. Pia, wasimamizi wote wa utekelezaji wa mtaala na wadau wengine wa elimu ya ualimu nchini watahakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

**Kamishna wa Elimu**

# Sehemu ya Kwanza

## Utangulizi

### 1.1. Usuli

Mifano mbalimbali duniani imeonesha kwamba ujenzi wa mfumo bora wa elimu unategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa walimu wanaouendesha. Aidha, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akisisitiza juu ya umuhimu wa walimu, alisema kwamba "sera yoyote ya elimu, hata iwe nzuri kiasi gani, haiwezi kufanikiwa bila kuwa na walimu walioandaliwa vyema" (Nyerere, 1988). Mwalimu aliendelea kusisitiza kwamba walimu ndiyo waliotwishwa jukumu la kujenga taifa lenye mawazo na mitazamo sahihi kupitia kazi yao ya kurithisha maarifa na maadili kwa vizazi vipya. Kwa mantiki hiyo, ni wazi kwamba ili mabadiliko yoyote ya sera, mfumo na mitaala ya elimu yaweze kuleta tija iliyokusudiwa ni lazima walimu waandaliwe vyema. Aidha, ni dhahiri kwamba, ili mitaala itekelezwe kwa ufanisi, ni lazima kuwe na walimu wa kutosha wenye weledi, maadili na ari stahiki.

Kwa mantiki hiyo, serikali imefanya mabadiliko ya Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi ili kumwezesha mwalimu kuendana na mabadiliko katika Mtaala wa Elimu ya Msingi unaolenga kuwezesha ujifunzaji kwa wanafunzi ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, mabadiliko katika mafunzo ya ualimu yatawezesha kufikia malengo ya elimu yaliyotamkwa na Azimio la Dunia la Jomtien la mwaka 1990, Itifaki ya Dakar ya mwaka 2000 na lengo la nne la Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2015 pamoja na Tamko la Incheon 2015. Pia, *Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014* Toleo la Mwaka 2023 inasisitiza upatikanaji wa walimu mahiri ambao watawawezesha wanafunzi kujenga uwezo wa kujitegemea, kupenda na kufanya kazi, kujenga stadi za maisha na kuwa na mtazamo chanya ili kushiriki katika kuleta mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Vilevile, Mtaala huu umejikita katika Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea iliyoasisiwa mwaka 1967 na Baba wa Taifa Mwalimu J. K. Nyerere inayosisitiza utoaji wa elimu inayomwezesha Mtanzania kujitegemea na kumudu maisha yake ya kila siku.

Kwa kuzingatia matamko hayo, sera, falsafa pamoja na maoni ya wadau, mtaala huu umeandaliwa kwa lengo la kumwandaa mwalimu mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya taifa kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia na mahitaji ya Karne ya 21. Mtaala huu pia, umelenga kuwaandaa walimu wenye ujuzi utakaowawezesha kujitegemea na kutumia vyema fursa zinazopatikana

nchini zitakazowawezesha kumudu maisha yao ya kila siku, kujiajiri au kuajiriwa. Aidha, mtaala huu unakidhi mahitaji ya ujenzi wa umahiri unaojumuisha uwezo wa kuwasiliana, kushirikiana, kufikiri kiyakinifu na kutumia stadi za ufundi, maisha na TEHAMA kuvumbua na kubuni mbinu na nyenzo anuai za kutatua changamoto za kiuchumi na kijamii.

**1.2 Muundo wa Elimu ya Ualimu Elimu ya Msingi**

Kama inavyoelekezwa na *Sera ya Elimu na Mafunzo 2014* Toleo la Mwaka 2023, Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi yatakuwa ni ya miaka miwili (2) kwa wahitimu waliomaliza Kidato cha Sita ambao watajiunga na mafunzo hayo kulingana na michepuo waliyosomea. Aidha, walimu waliohitimu Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali, Msingi na Maalumu wataruhusiwa kujiunga na mafunzo hayo kwa muda wa miaka miwili (2). Kwa upande wa wahitimu wa Kidato cha Nne wenye ufaulu wa Daraja I-III kwa kiwango cha alama “C” katika masomo matatu ambayo ni Basic Mathematics, Biology, Chemistry, Physics, Information and Computer Studies na Computer Science wataruhusiwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu kwa Ngazi ya Stashahada kwa muda wa miaka mitatu (03).

Walimu tarajali watasoma masomo ya utaalamu, masomo ya jumla na masomo ya mbinu za ufundishaji wa masomo ya Elimu ya Msingi. Masomo ya utaalamu yatahusisha Falsafa na Maadili ya Ualimu, Saikolojia na Sosholojia ya Elimu, Mitaala na Ufundishaji, Upimaji na Tathimini na Ualimu kwa Vitendo. Aidha, masomo ya jumla ni Elimu Jumuishi na Mawasiliano ya Kitaalamu kwa Mwalimu. Vilevile, masomo ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji itahusisha Lugha, Hisabati, Sayansi, Sayansi Jamii na Michezo na Sanaa. Mafunzo haya yanalenga kuwandaa walimu tarajali watakaofundisha wanafunzi wa Elimu ya Msingi. Sifa za wahitimu kujiunga na mafunzo na utaratibu mwingine wa utoaji na uendeshaji wa mafunzo haya utatolewa na wizara yenye dhamana kwa kushirikiana na taasisi husika.

# Sehemu ya Pili

## Dira, Malengo na Umahiri wa Jumla

Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi umezingatia dira ya elimu, malengo makuu ya elimu nchini Tanzania, malengo ya elimu ya ualimu na umahiri unaotarajiwa kujengwa kwa mwalimu tarajali.

### 2.1 Dira

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo katika kuleta maendeleo endelevu ya kitaifa na kimataifa.

### 2.2 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ambazo ni utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

### 2.3 Malengo ya Elimu ya Ualimu

#### 2.3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga

Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 2.3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo mahususi ya elimu ya ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-based research*).

## 2.4 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi unalenga kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;

(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;

(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*); na

(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani *classroom-based research*).

# Sehemu ya Tatu

## Maudhui ya Mtaala

Sehemu hii inafafanua maeneo ya ujifunzaji, masomo, umahiri mkuu na umahiri mahususi kwa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi ambayo yamebainishwa katika Jedwali Na. 3.1

**Jedwali Na.3.1:** *Maeneo ya Ujifunzaji, Masomo, Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi.*

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| Misingi ya Kinadharia | 1. Falsafa na Maadili ya Ualimu | 1.1 Kumudu falsafa na maadili ya ualimu | 1.1.1 Kuchambua falsafa na misingi ya elimu<br>1.1.2 Kutambua maadili, wajibu na haki za mwalimu wa Elimu ya Msingi |
| | 2. Saikolojia na Sosholojia ya Elimu | 2.1 Kumudu saikolojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 2.1.1 Kumudu misingi ya saikolojia ya elimu<br>2.1.2 Kuchambua hatua za makuzi na maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji<br>2.1.3 Kumudu nadharia na kanuni za ujifunzaji<br>2.1.4 Kumudu stadi za ushauri na unasihi kwa wanafunzi |
| | | 2.2 Kumudu sosholojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 2.2.1 Kumudu misingi ya sosholojia ya elimu<br>2.2.2 Kuchambua masuala ya kijamii yanayoathiri malezi na ujifunzaji |
| | 3. Mitaala na Ufundishaji | 3.1 Kumudu Mtaala wa Elimu ya Msingi | 3.1.1 Kuchambua Mtaala wa Elimu ya Msingi na vifaa vyake<br>3.1.2 Kuchambua masuala mtambuka katika elimu |

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 3.1.3 Kutafsiri mtaala katika programu ya ufundishaji na ujifunzaji |
| | 4. Upimaji na Tathmini | 4.1 Kumudu misingi ya upimaji na tathmini katika Elimu ya Msingi | 4.1.1 Kuchambua mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>4.1.2 Kumudu mbinu za kuandaa zana za upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri |
| | | 4.2 Kutumia matokeo ya upimaji kutathmini maendeleo ya mwanafunzi | 4.2.1 Kumudu mbinu za kutoa afua stahiki katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji |
| Masomo ya Jumla | 5. Elimu Jumuishi | 5.1 Kumudu misingi ya Elimu Jumuishi | 5.1.1 Kuchambua dhana ya Elimu Jumuishi<br>5.1.2 Kumudu mbinu za kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji<br>5.1.3 Kumudu mbinu za kutoa afua stahiki kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu katika ujifunzaji |

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | 5.2 Kumudu misingi ya kuwezesha ujifunzaji wa kila mwanafunzi katika mazingira jumuishi | 5.2.1 Kumudu matumizi ya mbinu na zana zinazozingatia mahitaji ya ujifunzaji ya kila mwanafunzi |
| Lugha na Mawasiliano | 6 Mawasiliano ya Kitaalamu kwa walimu | 6.1 Kumudu kuwasiliana kitaalamu | 6.1.1 Kuwasilisha taarifa za kitaaluma darasani kwa kutumia lugha stahiki<br>6.1.2 Kuwasilisha taarifa za kitaalamu nje ya darasa kwa kutumia lugha stahiki<br>6.1.3 Kutumia lugha stahiki kutengeneza mazingira wezeshi ya ujifunzaji<br>6.1.4 Kujenga tabia ya kusikiliza kwa umakini na kwa kujali<br>6.1.5 Kuwasiliana kwa ufanisi kwa kutumia Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT) |
| Mbinu za ufundishaji | 7 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Masomo ya Lugha | 7.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha katika Elimu ya Msingi | 7.1.1 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusikiliza kulingana na ngazi ya darasa husika<br>7.1.2 Kumudu mbinu za kufundisha matamshi kwa kuzingatia ngazi husika<br>7.1.3 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kuzungumza kwa kuzingatia ngazi husika |

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 7.1.4 Kumudu mbinu za kufundisha msamiati<br>7.1.5 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za kusoma kwa kuzingatia ngazi husika<br>7.1.6 Kumudu mbinu za kufundisha stadi za uandishi kwa kuzingatia ngazi husika<br>7.1.7 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji<br>7.1.8 Kumudu mbinu za kufundisha sarufi kwa kuzingatia ngazi husika<br>7.1.9 Kumudu matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa lugha nje ya darasa |
| | 8 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sayansi | 8.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sayansi katika Elimu ya Msingi | 8.1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa nadharia, uchunguzi na majaribio ya kisayansi<br>8.1.2 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Sayansi<br>8.1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sayansi nje ya darasa |

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
| --- | --- | --- | --- |
| | | 8.2 Kumudu matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 8.2.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa namna ya kubuni programu sahili za TEHAMA |
| | 9 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Hisabati | 9.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Hisabati katika Elimu ya Msingi | 9.1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa dhana ya namba<br>9.1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa vipimo, maumbo na aljebra<br>9.1.3 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Hisabati<br>9.1.4 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa takwimu na fedha<br>9.1.5 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Hisabati nje ya darasa |
| | 10 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira | 10.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira katika Elimu ya Msingi | 10.1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ramani<br>10.1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mfumo wa jua |

| **Maeneo ya Ujifunzaji** | **Masomo** | **Umahiri Mkuu** | **Umahiri Mahususi** |
|---|---|---|---|
| | | | 10.1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa sura ya nchi, rasilimali na matumizi yake<br>10.1.4 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira<br>10.1.5 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uhusiano kati ya mtawanyiko wa watu na matumizi ya rasilimali<br>10.1.6 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utunzaji wa mazingira na tabianchi<br>10.1.7 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira nje ya darasa |
| | 11 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili | 11.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili katika Elimu ya Msingi | 11.1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ulinzi wa historia, urithi na maadili ya Tanzania |

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | | | 11.1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maarifa ya jamii inayomzunguka<br>11.1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ushirikiano baina ya jamii za Kitanzania katika kujenga uhusiano wa kijamii na kiuchumi<br>11.1.4 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni<br>11.1.5 Kumudu ufaraguzi na matumizi ya teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili<br>11.1.6 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maendeleo na maadili ya jamii za Kitanzania wakati na baada ya ukoloni |
| | | | 11.1.7 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa historia na maadili ya ujenzi wa taifa katika kipindi cha 1961 hadi sasa<br>11.1.8 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili nje ya darasa |

| Maeneo ya Ujifunzaji | Masomo | Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|---|---|
| | 12 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sanaa na Michezo | 12.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sanaa na Michezo katika Elimu ya Msingi | 12.1.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uigizaji<br>12.1.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uimbaji na upigaji ala za muziki<br>12.1.3 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa uchoraji<br>12.1.4 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa ufinyanzi<br>12.1.5 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa utengenezaji wa vitu mbalimbali kwa kutumia makunzi<br>12.1.6 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mazoezi ya viungo<br>12.1.7 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa michezo |
| | | 12.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa na mashindano ya michezo | 12.2.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa maonesho na maonyesho ya sanaa<br>12.2.2 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa mashindano ya michezo |
| Ualimu kwa Vitendo | 13 Ualimu kwa Vitendo | 13.1 Kumudu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu ya Msingi | 13.1.1 Kuchambua mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Elimu ya Msingi |

| **Maeneo ya Ujifunzaji** | **Masomo** | **Umahiri Mkuu** | **Umahiri Mahususi** |
|---|---|---|---|
| | | 13.2 Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu ya Msingi | 13.2.1 Kuandaa mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji<br>13.2.2 Kuandaa zana za ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>13.2.3 Kuandaa darasa salama, changamshi na jumuishi |
| | | 13.3 Kuwezesha ujifunzaji wa mwanafunzi katika Elimu ya Msingi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | 13.3.1 Kutumia mbinu, teknolojia na vifaa vingine saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>13.3.2 Kuchopeka masuala mtambuka katika ufundishaji na ujifunzaji<br>13.3.3 Kuchopeka TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji<br>13.3.4 Kusimamia darasa katika ufundishaji na ujifunzaji<br>13.3.5 Kutumia mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa darasa kubwa katika mazingira jumuishi |
| | | | 13.3.6 Kuratibu shughuli za ujifunzaji nje ya darasa<br>13.3.7 Kupima, kutathmini na kutoa mrejesho wa maendeleo ya ujifunzaji wa mwanafunzi kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri<br>13.3.8 Kutoa ushauri na unasihi katika ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi |

# Sehemu ya Nne

## Ufundishaji na Ujifunzaji

Mtaala huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumwezesha mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Aidha, mkufunzi atatumia mbinu shirikishi za ujifunzaji zinazolenga kujenga umahiri uliokusudiwa kwa mwalimu tarajali kwa kuzingatia mahitaji anuai na uwezo wake. Mbinu hizo ni pamoja na zile zinazomwezesha mwalimu tarajali kufikiri, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni ziara za kimasomo, nyimbo, hadithi, changanyakete, kisamafunzo, majadiliano katika vikundi, kazi za vitendo, kazimradi, utafiti, majaribio ya kisayansi na nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

Masuala mtambuka yatafundishwa kwa kuyachopeka wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji katika masomo bebezi kwa kuzingatia uhusiano kati ya suala mtambuka na umahiri unaotarajiwa kujengwa. Masuala mtambuka hayo ni pamoja na elimu jumuishi, elimu ya jinsia, elimu ya amani, maadili, haki na wajibu wa mtoto. Pia, masuala mtambuka mengine ni haki za binadamu, ulinzi na usalama, usalama barabarani, elimu ya fedha, elimu ya rushwa na masuala ya muungano.

### 4.1 Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo Chuoni na Shule Jirani

Mwalimu tarajali anapaswa kushiriki katika mazoezi ya kufundisha kwa kushirikiana na wenzake. Mazoezi haya yanalenga kumwezesha mwalimu tarajali kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo kama vile haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini wanafunzi. Vitendo hivyo vitafanyika chini ya uangalizi wa karibu wa mkufunzi wake kwa lengo la kumpatia mrejesho utakaomwezesha kuboresha umahiri wake darasani.

Aidha, mwalimu tarajali anapaswa kushiriki katika:

(a) Mazoezi ya ufundishaji kupitia onesho au igizo ndani ya darasa lao katika ngazi ya chuo; na

(b) Ufundishaji wa kipindi kimoja katika shule iliyopo jirani na mazingira ya chuo chini ya uangalizi wa mwalimu husika wa somo au mkufunzi. Mazoezi ya ufundishaji kwa vitendo yatakuwa endelevu kwa muda wote wa mafunzo.

### 4.2. Rasilimali za Utekelezaji wa Mtaala

Mahitaji ya utekelezaji wa mtaala huu yanahusisha rasilimali watu, vitu, fedha na miundombinu. Viwango na sifa stahiki za rasilimali hizi zitatolewa na wizara yenye dhamana kupitia miongozo mbalimbali. Aidha, baadhi ya rasilimali za utekelezaji wa mtaala huu zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

#### 4.2.1 Rasilimali watu

Rasilimali watu inajumuisha walimu tarajali, wakufunzi na watumishi mwega:

**(a) Mwalimu tarajali**

Mwalimu tarajali ndiye mlengwa mkuu katika mtaala huu. Mwalimu tarajali anatakiwa kuwa na ufaulu wa kiwango cha daraja la I hadi la III katika mtihani wa taifa wa Kidato cha Sita ili aweze kujiunga na Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi. Pia, mafunzo yatawahusisha walimu wenye Astashahada ya Ualimu ya Awali, Msingi na Maalumu.

**(b) Mkufunzi**

Ili kuweza kutekeleza mtaala huu kwa ufanisi, mkufunzi atapaswa kuwa angalau na Shahada ya Umahiri katika masomo ya ualimu na uzoefu wa kufundisha usiopungua miaka miwili katika ngazi inayohusika. Hii ina maana kwamba, kwa mfano, mkufunzi anayetekeleza mafunzo ya ualimu wa Elimu ya Msingi anapaswa kuwa na uzoefu wa kufundisha katika shule ya msingi kwa muda wa miaka miwili au zaidi. Sifa hizi zitamwezesha kuwa mkufunzi bora kwani atakuwa anafahamu mazingira halisi ambayo mwalimu tarajali atakwenda kufanya kazi.

**(c) Watumishi mwega**

Watumishi mwega ni watumishi waendeshaji wasiokuwa wakufunzi. Watumishi hawa ni kiungo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mtaala huu. Kundi hili linajumuisha wataalamu kama vile wakutubi, wataalamu wa maabara, matabibu na wauguzi, makatibu muhtasi, wasaidizi wa ofisi na wengine. Wafanyakazi hawa watapaswa kuwa wamepata mafunzo katika chuo kinachotambulika na serikali na wamefuzu katika fani inayohusika.

#### 4.2.2 Rasilimali vitu na fedha

Utekelezaji fanisi wa mtaala huu unahitaji rasilimali vitu kama vile, ardhi, samani na miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Rasilimali hizo zinapaswa kuwa za kutosha na zinazokidhi viwango vya ubora vilivyobainishwa katika miongozo mbalimbali ya WyEST. Aidha, rasilimali hizo zinapaswa kuzingatia mahitaji ya wanachuo wote wakiwamo wenye mahitaji maalumu. Vilevile, upatikanaji wa rasilimali fedha ni muhimu katika uratibu na utekelezaji wa mtaala huu. Rasilimali fedha itapatikana kupitia uchangiaji wa fedha na mali kutoka kwa wadau mbalimbali.

### 4.2.3 Rasilimali muda

Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi yatakuwa ya muda wa miaka miwili (2) yenye jumla ya mihula minne (4). Siku za mafunzo kwa mwaka ni 194 ambazo ni sawa na wiki 39. Muda wa kusoma utakuwa ni saa 6 kwa siku na muda wa kipindi utakuwa saa moja. Hivyo kutakuwa na vipindi 6 kwa siku na vipindi 30 kwa wiki. Mwaka wa kuanza masomo utapangwa na Wizara yenye dhamana. Jedwali Na 4.1 linaonesha idadi ya vipindi kwa wiki na kwa muhula katika masomo yote yatakayofundishwa.

**Jedwali Na. 4. 1:** *Mchanganuo wa muda wa mafunzo kwa masomo ya utaalamu na ya jumla*

| Na. | Masomo | Idadi ya Saa Kwa Shughuli Zote | Shughuli za Mwaka wa Kwanza | | Shughuli za Mwaka wa Pili | | Vipindi kwa wiki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Muhula I | Muhula II | Muhula I | Muhula II | |
| 1 | Elimu Jumuishi | 70 | 35 | 35 | 0 | 0 | 2 |
| 2 | Mawasiliano ya Kitaalamu kwa Mwalimu | 140 | 50 | 50 | 20 | 20 | 2 |
| 3 | Falsafa na Maadili ya Ualimu | 70 | 35 | 35 | 0 | 0 | 2 |
| 4 | Saikolojia na Sosholojia ya Elimu | 140 | 50 | 50 | 20 | 20 | 2 |
| 5 | Mitaala na Ufundishaji | 70 | 35 | 35 | 0 | 0 | 2 |
| 6 | Upimaji na Tathmini | 140 | 50 | 50 | 20 | 20 | 2 |
| 7 | Elimu ya Dini | 70 | 25 | 25 | 10 | 10 | 1 |

| Na. | Masomo | Idadi ya Saa Kwa Shughuli Zote | Shughuli za Mwaka wa Kwanza | | Shughuli za Mwaka wa Pili | | Vipindi kwa wiki |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Muhula I | Muhula II | Muhula I | Muhula II | |
| 8 | Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia Somo 1 | 350 | 150 | 150 | 30 | 20 | 5 |
| 9 | Mbinu za ufundishia na ujifunzia Somo 2 | 350 | 150 | 150 | 30 | 20 | 5 |
| 10 | Ualimu kwa Vitendo | 490 | 100 | 120 | 190 | 80 | 7 |
| | | **1,890** | **680** | **700** | **320** | **190** | **30** |

**Jedwali Na. 4.2:** *Mchanganuo wa Muda wa Mafunzo kwa Masomo ya Kufundishia*

| Na | Mchepuo | Masomo | Idadi ya Vipindi kwa Wiki | Muda wa Mafunzo kwa Mihula ya Masomo | | | | Idadi ya Saa Kwa Shughuli Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka wa kwanza | | Mwaka wa Pili | | |
| | | | | Muhula I | Muhula II | Muhula I | Muhula II | |
| 1 | Lugha | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| | | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiarabu | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| | | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Kichina | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |

| Na | Mchepuo | Masomo | Idadi ya Vipindi kwa Wiki | Muda wa Mafunzo kwa Mihula ya Masomo | | | | Idadi ya Saa Kwa Shughuli Zote |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwaka wa kwanza | | Mwaka wa Pili | | |
| | | | | Muhula I | Muhula II | Muhula I | Muhula II | |
| | | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Kifaransa | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| | | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiingereza | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| 2 | Hisabati | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Hisabati | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| 3 | Sayansi | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sayansi | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| 4 | Sayansi Jamii | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Jiografia na Mazingira | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| | | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Historia ya Tanzania na Maadili | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |
| 5 | Sanaa na Michezo | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji wa Sanaa na Michezo | 5 | 150 | 150 | 30 | 20 | **350** |

### 4. 3 Lugha ya kufundishia na kujifunzia

*Sera ya Elimu na Mafunzo 2014* Toleo la Mwaka 2023 inatamka kuwa lugha za Kiswahili na Kiingereza zitatumika kufundishia na kujifunzia katika ngazi ya Stashahada ya Elimu Ualimu. Hivyo, Kiswahili kitatumika kama lugha ya kufundishia kwa walimu tarajali wanaoandaliwa kufundisha shule zinazotumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza kitatumika kama lugha ya kufundishia kwa walimu tarajali wanaoandaliwa kufundisha shule zinazotumia lugha ya Kiingereza.

### 4.4 Ushiriki wa Wadau katika Utekelezaji wa Mtaala wa Stashahada ya Ualimu-Elimu ya Msingi

Ushirikishwaji wa wazazi/walezi na wadau wengine wa elimu ni muhimu sana katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa mwalimu tarajali. Wadau hawa wamekuwa na mchango mkubwa katika kufanikisha utekelezaji wa mitaala nchini. Vyuo vya Ualimu havina budi kushirikiana vyema na wadau hawa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika utoaji wa Elimu ya Ualimu.

### 4.5 Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mtaala wa Stashahada ya Ualimu-Elimu ya Msingi

Usimamizi wa utekelezaji wa Mtaala wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu ni hatua muhimu ya kuhakikisha kuwa malengo yake yametekelezwa kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa. Mtaala huu utasimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia ofisi ya Kamishna wa Elimu Kitengo cha Elimu ya Ualimu ambacho kina jukumu la kuratibu programu za mafunzo ya ualimu. Usimamizi wa mtaala ngazi ya chuo utafanywa na Mkuu wa Chuo kwa kushirikiana na Bodi ya Chuo, Maofisa Elimu Mkoa, Wilaya na Wathibiti Ubora wa elimu wa Kanda na Wilaya.

Aidha, ufuatiliaji wa Mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Ualimu unalenga kuona au kupata mrejesho wa namna mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unavyofanyika ukihusisha mafanikio, changamoto na namna ya kuzitatua ili kupata matarajio yaliyokusudiwa. Hivyo, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mtaala huu utafanywa na wizara inayohusika yenye dhamana kwa kushirikiana na taasisi zinazosimamia na kuratibu mafunzo ya ualimu.

# Sehemu ya Tano

## Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Mtaala huu utatumia mfumo wa upimaji unaozingatia vigezo vinavyotambulika vya upimaji wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa maendeleo ya kila siku ya mwalimu tarajali na mitihani ya mwisho ya kukamilisha ngazi inayohusika. Upimaji wa ndani utaratibiwa chuoni wakati wa ufundishaji na ujifunzaji na upimaji wa nje utaratibiwa na mamlaka inayohusika. Mbinu mbalimbali za upimaji zitatumika kupima nadharia na vitendo katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji. Mbinu hizo ni pamoja na bunguabongo, uchunguzi, majaribio, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo na kazimradi. Mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mitihani ya mwisho kulingana na sababu ya upimaji, mahitaji ya somo, mahitaji anuai ya mwanafunzi na umahiri unaokusudiwa kujengwa. Aidha, mtaala unasisitiza kutumia baadhi ya zana za upimaji kama vile orodhahakiki, dodoso, mkoba wa kazi na fomu za maendeleo ya ujifunzaji wa mwalimu tarajali.

Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji. Kwa upande wa upimaji endelevu, mchanganuo wa alama katika masomo ya Ualimu kwa Vitendo na Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa masomo ya ngazi inayohusika itakuwa asilimia sabini (70%) ambapo Mtihani wa Muhula wa Pili kwa Mwaka wa Kwanza ni asilimia kumi (10%), kazimradi ya ufaraguzi ni asilimia kumi na tano (15%), ufundishaji igizi (kiduchu) asiliamia ishirini (20%) na ufundishaji wa shule jirani itakuwa asilimia ishirini na tano (25%). Rejea **Jedwali Na 5.**1 linaloonesha mchanganuo wa alama za upimaji endelevu kwa masomo ya Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji na Ualimu kwa Vitendo.

Aidha, kwa upande wa masomo ya utaalamu na ya jumla, mchanganuo wa alama za upimaji endelevu utakuwa kama ifuatavyo; Mtihani wa Muhula wa Kwanza kwa Mwaka wa Kwanza ni asilimia sita (6%), Mtihani wa Muhula wa Pili kwa Mwaka wa Kwanza ni asilimia sita (6%), Mtihani wa Muhula wa Kwanza kwa Mwaka wa Pili ni asilimia sita (6%), Mkoba wa kazi itakuwa asilimia tano (5%) na Kazimradi itakuwa asilimia saba (7%). Rejea **Jedwali Na 5.2** linaloonesha mchanganuo wa alama za upimaji endelevu kwa masomo ya utaalamu na ya jumla.

**Jedwali Na. 5.1:** *Alama za upimaji endelevu kwa masomo ya Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji na Ualimu kwa Vitendo.*

| Na. | Shughuli ya Upimaji | % |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhala wa Pili Mwaka wa Kwanza | 10 |
| 2 | Kazi Mradi Ufaraguzi | 15 |
| 3 | Ufundishaji Igizi/Kiduchu | 20 |
| 4 | Ufundishaji Shule Jirani | 25 |
| | **Jumla** | **70** |

**Jedwali Na. 5.2:** *Alama za upimaji endelevu kwa masomo ya utaalamu na ya jumla.*

| Na. | Shughuli ya Upimaji | % |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa I kwa Mwaka wa I | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Muhula wa II kwa Mwaka wa I | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Muhula wa I kwa Mwaka wa II | 6.0 |
| 4 | Kazi Mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

**TANBIHI:** Kwa masomo yatakayoishia Mwaka wa Kwanza kama vile Elimu Jumuishi, Falsafa na Maadili na Mitaala na Ufundishaji, Upimaji endelevu utaendelea kufanyika hadi Mwaka wa Pili ili kuwaandaa walimu tarajali kwa ajili ya mtihani wa kuhitimu mafunzo.

# Bibliografia


Ministry of Education, Science and Technology. (2019). *National curriculum framework for basic and teacher education*. Tanzania Institute of Education.

National Bureau of Statistics. (2008). *National panel survey* 2008-2009 - *Disability rates.* National Bureau of Statistics.

National Bureau of Statistics. (2008). *Tanzania disability survey report* 2008. National Bureau of Statistics.

National Bureau of Statistics. (2019). *Voluntary national review* (vnr) 2019-*Empowering people and ensuring inclusiveness and equality*. National Bureau of Statistics.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Mtaala wa mafunzo ya astashahada ya ualimu*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Taarifa ya kikaokazi cha kujadili uboreshaji wa mafunzo ya ualimu ngazi ya astashahada*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2018). *Ripoti ya utafiti wa maoni ya kuboresha mtaala wa mafunzo ya ualimu tarajali ngazi ya astashahada*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2018). *Utoaji wa elimu ya awali.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2022). *Ripoti ya maoni ya wadau wa elimu kuhusu uboreshaji wa mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

United Republic of Tanzania. (2019). *National strategy on inclusive education* 2018-2021. Ministry of Education, Science and Technology.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2014). *Sera ya elimu na mafunzo.* Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.